Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye Maadhimisho ya Kumbukizi ya Hayati Rais Benjamin William Mkapa, Mlimani City 14 Julai, 2021

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Waheshimiwa Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; (Mzee Mwinyi, Mzee Kikwete na Mzee Karume)

Mheshimiwa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar

Mama Anna Mkapa; Mjane wa Mpendwa wetu Hayati Rais Benjamin William Mkapa;

Mwenyekiti wa Bodi ya Benjamin William Mkapa (Dr. Kimambo)

Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Benjamin Mkapa (Dr. Ellen Mkondya Senkoro)

Jumuiya ya Wanadiplomasia;

Washiriki kutoka Sekta Binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali;

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Taasisi ya Benjamin William Mkapa;

Familia na Marafiki;

Mabibi na Mabwana;

Ninayo furaha kujumuika nanyi asubihi ya leo katika maadhimisho haya ya safari ya maisha na urithi wa Mpendwa wetu, Hayati Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu na Mwanzilishi wa Taasisi ya Benjamin William Mkapa.

Nakushukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini kwa kunialika kwenye shughuli hii adhimu. Awali ya yote nikupongeze wewe na Bodi unayoiongoza kwa kuazimia kuadhimisha Kumbukumbu hii mwaka huu na miaka ijayo. Pili, niwapongeze kwa maandalizi mazuri ya Maadhimisho haya ambayo hapana shaka yamefana sana. Binafsi, nimefurahishwa sana na namna maadhimisho haya yalivyoratibiwa. Nimesikiliza shuhuda zilizotolewa na jopo la wataalam lililojadili agenda muhimu ya 'Afya kwa Wote'. Itapendeza, miaka ijayo kufanya maadhimisho haya kule Zanzibar. Serikali yangu itawapatia kila aina ya ushirikiano mtakaouhitaji.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Nilipopokea mwaliko huu, sikusita hata kidogo kuukubali, na nikalazimika kuahirisha shughuli nyingine ili niweze kuwepo hapa leo. Nilifanya hivyo kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, Hayati Rais Mstaafu Benjamin Mkapa kwangu mimi alikuwa ni zaidi ya kiongozi. Alikuwa ni Rais wangu na alinipa fursa ya kuhudumu katika serikali yake kwa nafasi ya Naibu Waziri kwa miaka 5. Alikuwa ndio Rais wa kwanza aliyefungua safari yangu ya kisiasa pale aliponiteua kuwa Naibu Waziri mwaka 2000. Aliwekeza kwangu imani kubwa na alibeba dhamana kubwa sana kuniteua mimi wakati huo nikiwa kijana na mgeni kabisa kwenye siasa nikitokea katika taaluma ya udaktari. Kupitia mikono yake ya ulezi, alinilea, nikakua kufika hapa nilipo leo. Nasikitika tu kuwa aliondoka

kabla ya kushuhudia nikiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar. Sina shaka angejivunia sana kuona matunda ya kazi ya ulezi wake.

Hayati Rais Mkapa kwangu pia alikuwa ni baba, naye alinichukulia kama mwanawe. Wakati wote alinipatia fursa ya kumuona na kuvuna hekima na busara zake akiwa madarakani na hata baada ya kustaafu. Kwa kweli nimefaidika naye sana. Kwake nimejifunza uongozi, nimejifunza kuhudumu na nimejifunza nidhamu ya kazi. Daima nilimjua kama kiongozi mwenye maono, hofu ya Mungu na mwanazuoni. Nilifurahia sana mazungumzo yangu naye na daima niliagana nae nikiwa nimechota busara kutoka kwake.

Pili, mimi ni mmoja wa wadau wa Taasisi ya Benjamin William Mkapa. Nilipata fursa ya kuhudumu katika Taasisi hii kwa nafasi ya Mwenyekiti wa kwanza wa Bodi ya Wadhamini nilipoteuliwa na Hayati Mzee Mkapa mwaka 2006. Uteuzi ule unathibitisha kile nilichosema awali ya kuwa, daima, alinipa imani na heshima kubwa sana. Nami niliamini sana katika maono, nia na azma yake ya kutaka kuona kila Mtanzania, popote alipo na katika hali yoyote ya kiuchumi aliyonayo, anapata huduma bora ya afya bila kizuizi. Alituhamasisha kuhakikisha kuwa tunabuni mipango, mbinu na mikakati yenye kutafuta majibu juu ya changamoto zinazozuia huduma bora za afya kuwafikia wahitaji huko waliko zikiwemo, ukosefu wa nyumba za watumishi na ukosefu wa watumishi wa kada mbalimbali za afya. Nafurahi kuwa nilitimiza wajibu wangu huo ipasavyo na najivunia fursa ile. Ninapoona Taasisi hii imefikisha miaka 15, ninafarijika na kujivunia kuwa sehemu ya mafanikio yake ambayo yaliyolezewa kwa kina mapema leo.

Mheshimiwa Rais, Mabibi na Mabwana;

Hayati Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa ameifanyia nchi yetu mambo makubwa. Mageuzi ya kiuchumi na yasoko aliyoyaongoza yamekuwa na mchango mkubwa kwa Zanzibar. Yalisaidia sana kuifungua Zanzibar kutoka katika ukiritimba wa uchumi wa karafuu (Clove Monoculture).

Nia yake njema na kujali kwake kulichangia sana kupatikana kwa Muafaka wa kwanza wa kisiasa Zanzibar ambao ulirejesha hali ya amani na utulivu. Muafaka ule ulisaidia sana kutuliza joto la kisiasa Zanzibar na kufungua fursa za majadiliano na mashirikiano ya kisiasa visiwani kwetu. Msimamo wake juu ya Muungano ulikuwa thabiti, usioyumba, na alikuwa tayari kuusimamia na kuulinda Muungano wetu kwa kauli na vitendo.

Zanzibar pia ni mnufaikaji mkubwa wa miradi ya Taasisi ya Benjamin Mkapa tokea mwaka 2007. Miradi hiyo imejikita katika sekta ya afya hususan kujenga uwezo wa watumishi wa afya katika kutoa huduma zinazohusu VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na Afya ya Mama na Mtoto. Tunajivunia mafanikio yaliyopatikana kupitia miradi hii ambayo kwa kweli imesaidia sana juhudi za Serikalia ya Mapinduzi ya Zanzibar kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wote.

Napata faraja kuwa mazungumzo ya mashirikiano kati ya Serikali ninayoiongoza na Taasisi ya Benjamin William Mkapa yako katika hatua nzuri. Ni matumaini yetu kuwa yakikamilika, yatasaidia sana kufanikisha azma yetu ya kupunguza uhaba wa watumishi wa sekta ya afya, pamoja na upatikanaji wa fedha za kuwezesha lengo la Serikali ninayoiongoza kumpatia bima ya afya kila Mzanzibari (Universal Health Insurance). Nawahakikishia ushirikiano wangu na wa wenzangu wote Serikalini kufanikisha azma hii.

Nimeguswa pia na uamuzi wenu wa kuanzisha Mfuko wa Wakfu wa Benjamin William Mkapa kwa ajili ya kuendeleza kazi zake kupitia Taasisi yenu. Ni wazo sahihi kwa wakati sahihi. Wakfu hii ikifanikiwa, itasaidia sana kupunguza utegemezi wa misaada na kujenga uwezo wa Taasisi kujitegemea. Daima, kujitegemea ndio ilikuwa nadhiri ya Hayati Rais Mkapa.

Mheshimiwa Rais, Mabibi na Mabwana;

Sisi Zanzibar tunatekeleza Dira ya Maendeleo ya 2050 ambayo inalenga kuifikisha Zanzibar kuwa nchi ya Uchumi wa Kati wa Juu (Upper Middle-Income Status) ifikapo mwaka 2050. Dira hiyo imejengwa kwenye nguzo nne ambazo ni *Mapinduzi ya Kiuchumi, Rasilimali Watu na Huduma za Jamii, Utawala Bora na Uhimilivu, na Miundombinu.*

Kuhusu Rasilimali Watu na Huduma za Jamii, tumedhamiria kujenga jamii ya watu wenye afya bora, wenye kuweza kushindana na wengine duniani, wabunifu na wachapakazi ili waweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa nchi. Ili kufikia lengo hilo, hatuna budi

kuhakikisha kuwepo kwa huduma za jamii zilizo bora, za uhakika na zenye kutumainika. Ni katika muktadha huu tunawakaribisha sana Taasisi ya Benjamin Mkapa tushirikiane kujenga mifumo ya kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya, ambazo zinafikiwa na wote, zinazotolewa na watoa huduma wenye sifa na zinazoendana na teknolojia ya kisasa. Tungependa kuona kile mlichofanya huku Bara hususan katika ujenzi wa mifumo ya afya, kifanyike pia na Zanzibar.

Mheshimiwa Rais, Mabibi na Mabwana;

Naomba nimalizie hotuba yangu kwa mara nyengine tena kuushukuru uongozi wa Taasisi ya Benjamin William Mkapa kwa heshima hii kubwa walionitunukia ya kuzungumza kwenye hadhara hii.

Naomba sasa nichukue furasa hii kukukaribisha ili uzungumze na hadhara hii.

Mheshimiwa Rais, Karibu!